TANGAZO LA SERIKALI NA. 548 la tarehe 4/8/2023

SHERIA YA UTHAMINI NA USAJILI WA WATHAMINI,

(SURA YA 138)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 64 (1))*

KANUNI ZA ADA KWA HUDUMA ZA UTHAMINI NA USHAURI WA KITAALAM ZA MWAKA 2023

MPANGILIO WA KANUNI

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
NAMNA YA UTOZAJI WA ADA KWA HUDUMA ZA UTHAMINI NA USHAURI WA KITAALAM

3. Ada kwa huduma za uthamini na ushauri wa kitaalam.
4. Uthamini wa sehemu ya mali.
5. Kutohusika kwa jengo chakavu, lililokarabatiwa au kubadilishwa.
6. Ada ya uthamini wa mali kwa maafikiano.
7. Uthamini kwa kusudi zaidi ya moja.
8. Ada ya uthamini wa mali tofauti za mteja mmoja.
9. Kodi.

SHERIA YA UTHAMINI NA USAJILI WA WATHAMINI,
(SURA YA 138)

**KANUNI**

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 64 (1))*

KANUNI ZA ADA KWA HUDUMA ZA UTHAMINI NA USHAURI WA KITAALAM ZA MWAKA 2023

## SEHEMU YAKWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1.-(1) Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Ada kwa Huduma za Uthamini na Ushauri wa Kitaalam za Mwaka 2023.

(2) Kanuni hizi zitatumika kwa Wathamini waliosajiliwa na kutoa huduma za uthamini na ushauri wa kitaalamu kwa sekta binafsi.

Tafsiri

2. Katika Kanuni hizi isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

Sura ya 138

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Uthamini na Usajili wa Wathamini;

"thamani" itakuwa na maana kama ilivyo tafsiriwa katika Sheria; na

"Wathamini waliosajiliwa" itakuwa na maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria.

## SEHEMU YA PILI
## NAMNA YA UTOZAJI WA ADA KWA HUDUMA ZA UTHAMINI NA USHAURI WA KITAALAM

Ada kwa huduma za uthamini na ushauri wa

3. Ada kwa huduma za uthamini na ushauri wa kitaalam zitakuwa kama ilivyoainishwa katika

kitaalam

Jedwali.

Uthamini wa sehemu ya mali

4. Endapo ni lazima kufanya uthamini wa mali yote kufikia thamani ya sehemu ya mali hiyo, malipo ya kuthamini sehemu ya mali itategemea ile ya uthamini wa mali yote ili mradi pande zote zinaweza kujadiliana juu ya ada itakayolipwa baada ya kuafikiana.

Kutohusika kwa jengo chakavu, lililokarabatiwa au kubadilishwa

5. Ada zilizoainishwa katika Jedwali hazijumuishi jengo chakavu, lililokarabatiwa au kubadilishwa.

Ada ya uthamini wa mali kwa maafikiano

6. Pale ambapo maelekezo yatatolewa kufanya utahamini wa baadhi ya mali kwa makubaliano sambamba na uthamini wa mali nyingine, ada ya uthamini itakuwa ya mapatano.

Uthamini kwa kusudi zaidi ya moja

7. Endapo mteja anahitaji kufanyiwa uthamini kwa kusudi zaidi ya moja, malipo yatakuwa mara moja na nusu ya malipo husika.

Ada ya uthamini wa mali tofauti za mteja mmoja

8. Endapo mthamini atafanya uthamini wa mali tofauti za mteja mmoja, ada itakuwa kwa thamani ya jumla ya mali zote.

Kodi

9. Ada zote za uthamini zilizoainishwa katika Jedwali hazitajumuisha kodi, gharama za usafiri au gharama za kurejeshewa, ada za upekuzi na ada za kupata vibali vya serikali; ada hizo zitakokotolewa na kutozwa tofauti.

## JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 3)*

ADA ZA UTHAMINI KWA UTHAMINI WA KITAALAM NA USHAURI ULIOFANYWA KWA SEKTA BINAFSI

| AINA YA MALI | MAKADIRIO YA THAMANI (TZS) | ADA YA UTHAMINI (TZS) | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| | | | |
| Aina zote za majengo | Milioni 100-300 | 600,000.00 | ukiondoa VAT na ada za Serikali |
| | Milioni 400-600 | 1,000,000.00 | ukiondoa VAT na ada za Serikali |
| | Milioni 700 – Bilioni 1 | 1,300,000.00 | ukiondoa VAT na ada za Serikali |
| | Zaidi ya bilioni 1 | ada haitakuwa chini 0.5% ya thamani ya soko | ukiondoa VAT na ada za Serikali |
| | | | |
| Samani za ofisi na vifaa, nguzo, hisa za biashara na vifaa vya majumbani vya kawaida, vifaa vya ofisi na vifaa vya TEHAMA | Milioni 100-250 | 700,000.00 | ukiondoa VAT na ada za Serikali |
| | Milioni 251-500 | 1,500,000.00 | ukiondoa VAT na ada za Serikali |
| | Milioni 600-Bilioni 1 | 2,000,000.00 | ukiondoa VAT na ada za Serikali |
| | Zaidi ya bilioni 1 | ada haitakuwa chini 0.5% ya thamani ya soko | ukiondoa VAT na ada za Serikali |
| | | | |
| Mitambo na mashine: pamoja na vifaa vinavyohamishika | Milioni 100-250 | 500,000.00 | ukiondoa VAT na ada za Serikali |
| | Milioni 300-600 | 1,000,000.00 | ukiondoa VAT na ada za Serikali |
| | Milioni 700-Bilioni 1 | 1,500,000.00 | |
| | Zaidi ya bilioni 1 | ada hazitakuwa chini 0.5% ya thamani ya soko | ukiondoa VAT na ada za Serikali |
| | | | |
| Magari, vyombo vya baharini na | Milioni 100-250 | 500,000.00 | ukiondoa VAT na ada za Serikali |

*Tangazo La Serikali Na. 548 (Linaendelea)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| ndege | Milioni 100-600 | 1,000,000.00 | ukiondoa VAT na ada za Serikali |
| | Milioni 700-Bilioni 1 | 1,500,000.00 | |
| | Zaidi ya bilioni 1 | ada haitakuwa chini 0.5%ya thamani ya soko. | ukiondoa VAT na ada za Serikali |

Dodoma,
2 Julai, 2023

CLETUS ELIGIUS NDJOVU
*Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili wa Wathamini*